602

# THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KPSEA 2025

## KISWAHILI

## Okt. 2025 - Muda: Saa 1

4943327

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 30. Jibu maswali yote.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
4. Tumia penseli ya kawaida (HB).
5. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

   **NAMBA YAKO YA TATHMINI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**

6. Kwa kila swali, 1 - 30, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A**, **B**, **C** na **D**. Herufi hizi zimeandikwa ndani ya viduara. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
7. Kwenye karatasi ya majibu, lionyeshe jibu sahihi kwa kujaza kiduara chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu, ukitumia penseli.
8. Usitie alama zozote nje ya viduara. **Thibitisha jibu lako kabla ya kujaza kiduara ulichochagua.**

   **Mfano**

   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **28.** Maneno haya yanastahili kuwa katika hali ya umoja pekee. Chagua jibu lenye maneno yasiyo katika hali ya umoja.

   A yai, dirisha, chandarua
   B uso, msusi, mwiko
   C ufagio, kiti, mswaki
   D kuni, vifutio, matunda

   Jibu sahihi ni D.

   **Katika karatasi ya majibu:**

   Katika viduara vinavyoonyesha majibu ya swali namba **28**, jaza kiduara chenye herufi **D** kwa kutumia penseli.

   **28.** (A) (B) (C) ●

9. Jaza kiduara chako vizuri, **KIWE CHEUSI** na alama zisijitokeze nje ya kiduara.
10. Kwa kila swali, jaza **kiduara kimoja tu** kati ya viduara vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 6 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa na maswali yote yapo ipasavyo.**

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

© 2025 The Kenya National Examinations Council



Geuza ukurasa

**Swali la 1 hadi la 5**

*Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.*

*(Ni jioni, shuleni. Maria ameketi kwenye fomu akisoma hadithi. Sara, rafikiye, anamjia kwa kunyatia.)*

**Sara**: (*Baada ya kumwamkua.*) Maria, ni hadithi gani hiyo ambayo imeyateka nyara mawazo yako mpaka huoni mvua ikija?

**Maria**: (*Akitabasamu.*) Hata si hadithi. Ni yaliyomo katika hadithi yenyewe. Yanakuvuta tu bila kutaka.

**Sara**: (*Akimakinika zaidi.*) Kwani inahusu nini?

**Maria**: Inahusu jinsi urafiki wa Kuku na Mwewe ulivyofikia kikomo. (*Akicheka.*) Ni hali ya kusisimua na hapo hapo kuhuzunisha.

**Sara**: (*Akikubaliana naye.*) Ahaa! Sasa naelewa sababu ya kuzama huko hadithini. Hata mimi ningependa kuisoma ila naona mvua ya masika inatishia kuanguka. Ni muhimu tuondoke.

**Maria**: Kumbe! Sikuwa nimeona dalili ya mvua. Kweli, tunaweza kuondoka.

1. Kauli, 'Baada ya kumwamkua' imetumiwa katika mazungumzo. Unadhani Sara alitumia neno lipi kumwamkua Maria?
   A. Chewa
   B. Shikamoo
   C. Masalheri
   D. Hamjambo

2. Sara anakubaliana na Maria kwa kusema "Ahaa!" Sara alitumia ishara gani kuonyesha hali hii?
   A. Alitikisa kichwa.
   B. Alimpungia mkono.
   C. Alimkazia macho.
   D. Alimpigia makofi.

3. Mwishoni mwa mazungumzo, Maria na Sara wanaondoka. Sara angetumia neno lipi kumuaga Maria?
   A. Alamsiki
   B. Mchana mwema
   C. Baki salama
   D. Kwaheri

4. 'Ni muhimu tuondoke.' Sara angetumia maneno mengine yepi yenye adabu?
   A. Utasimama twende?
   B. Hebu simama.
   C. Bado umeketi?
   D. Inafaa twende.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

5. Sara anamtahadharisha Maria kwamba mvua inakaribia kunyesha. Maria anastahili kumwambia nini Sara?
   A. Kunradhi
   B. Asante
   C. Tafadhali
   D. Simile

**Swali la 6 hadi la 9**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Daudi alipenda sana kucheza kandanda. Kila alipouona mchezo huo ukichezwa karibu naye alifululiza hadi pahali hapo na kuomba kushirikishwa. Wakati mwingine alijitengenezea mpira kwa vitambaa vikuukuu na kuwaita wenzake wacheze pamoja.

Siku moja, Daudi alitumwa dukani kununua mkate na pakiti ya maziwa. Alipokuwa akirudi nyumbani, aliona marafiki wake wakicheza kandanda karibu na nyumbani kwao. Ghafla, kiu yake ya kandanda iliamka, akasahau mfuko wa bidhaa aliokuwa amebeba na kujitoma katika mchezo. Yeye na wenzake walizama katika kusakata gozi. Hakuna aliyemwona paka akinyemelea mfuko ambao Daudi alikuwa ameuweka karibu na lango.

Daudi hakujua vipi, lakini baada ya muda, moyo ulimwambia autazame ule mfuko. Lo! Alimwona paka mkubwa ameining'iniza pakiti ya maziwa mdomoni. Daudi **alitoka shoti** kumfuata paka. Hata alipomfikia, pakiti ilikuwa tupu! Paka alikuwa amekamilisha kazi yake.

6. Kulingana na aya ya **kwanza**, Daudi
   A. alipenda kuchezea mpira karibu na kwao.
   B. alifurahia kutazama mechi ya kandanda ikiendelea.
   C. aliwauliza wengine wamshirikishe katika kandanda.
   D. aliwashauri wenzake watumie mpira wa vitambaa vikuukuu.

7. Daudi ni mbunifu kwa kuwa
   A. anang'amua kwamba alikuwa na mfuko.
   B. anacheza kandanda na wenzake nyumbani.
   C. anamfuata paka kuokoa maziwa.
   D. anajiundia vifaa vya kuchezea.

8. Daudi alifika nyumbani bila pakiti ya maziwa. Huenda alifanya mambo yafuatayo, **isipokuwa**:
   A. alisimulia kuhusu mchezo wa kandanda.
   B. aliomba msamaha kwa kosa alilofanya.
   C. alilia kwa kujutia aliyofanya.
   D. aliahidi kuwa makini zaidi.

9. Maana ya **'alitoka shoti'** ni
   A. aliweka mpira chini.
   B. aliwaaga wenzake.
   C. aliondoka haraka.
   D. aliuchukua mfuko wake.

**Swali la 10 hadi la 12**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Yusuf, Ali, Amina na Pendo huzingatia lishe bora. Pamoja na kula vyakula vyenye wanga na protini, wao hula mboga na matunda ili kupata vitamini. Jedwali lifuatalo linaonyesha matunda ambayo kila mmoja anakula kwa siku nne zilizoonyeshwa.

| | Jumatatu | Jumanne | Jumatano | Alhamisi |
|---|---|---|---|---|
| **Yusuf** | pera | zabibu | tikitimaji | embe |
| **Ali** | tikitimaji | tufaha | pera | zabibu |
| **Amina** | papai | papai | pera | tikitimaji |
| **Pendo** | embe | papai | zabibu | pera |

10. Ni matunda gani ambayo yanaliwa siku mbili tu?
   A. papai, zabibu
   B. papai, embe
   C. tufaha, papai
   D. tikitimaji, pera

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

**11.** Baadhi ya matunda yanaliwa mara nyingi kuliko mengine. Unadhani kwa nini hali ikawa hivyo? Matunda hayo

A. yanapatikana kwa wingi, yana bei nafuu.
B. yana rangi ya kuvutia, yanaiva haraka.
C. yanapendwa na wengi, ni makubwa.
D. yanastahimili kiangazi, ni matamu.

**12.** Maana ya **huzingatia** ni

A. hutofautisha vyema.
B. hufurahi kuona.
C. hueleza waziwazi.
D. hutilia maanani.

**Swali la 13 hadi la 15**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Baharini na maziwani mnaishi aina za samaki na wanyama wengine wengi. Wanyama hao wa majini wana umuhimu mkubwa kwa maisha ya binadamu kwa jumla. Kuna wale wanaotumiwa kama chakula, wanaosawazisha mazingira na hata wanaoipamba dunia tu. Kuna aina kadha za wanyama wa majini kama vile papa, nyangumi, dagaa na kambare. Bila kuwepo kwao binadamu atanyimwa sio tu chakula chenye madini bali pia burudani inayotokana na mienendo ya wanyama hao wawapo majini.

Baadhi ya wanyama wa majini ni wa ajabu. Mmoja wao ni papa. Papa anasemekana kwamba ndiye samaki mkubwa zaidi ulimwenguni. Ana ngozi ngumu, meno makubwa na hula watu! Wasemao husema ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni. Ikiwa umeshangazwa na ya papa kuwala watu, sikiliza ya nyangumi. Nyangumi ni mwenye kimo kikubwa. **Utafiti** unaonyesha kwamba anaweza kuwa na urefu wa futi tisini na uzani wa kilo elfu mia moja na hamsini. Nyangumi hunyonyesha vikembe vyake. Mataifa yanafaa, kuhakikisha kwamba uhai wa baharini unatunzwa kabla mambo yaende segemnege.

**13.** Kulingana na **aya ya kwanza,** wanyama wana umuhimu ufuatao **isipokuwa**

A. kuwa lishe kwa binadamu.
B. kufanya dunia ipendeze.
C. kufanya mazingira iwe sawa.
D. kuwala wanyama wengine.

**14.** Ni kauli ipi katika kifungu inayoonyesha kwamba baadhi ya tabia za nyangumi ni sawa na za mwanadamu?

A. Nyangumi ni mwenye kimo kikubwa.
B. Nyangumi hunyonyesha vikembe vyake.
C. Anaweza kuwa na urefu wa futi tisini.
D. Ana uzani wa kilo elfu mia moja na hamsini.

**15.** Kulingana na kifungu, neno lingine lenye maana sawa na **utafiti** ni

A. uvumbuzi.
B. utatuzi.
C. uchunguzi.
D. ugunduzi.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

**Swali la 16 hadi la 20**

*Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi* ***16*** *hadi* ***20****. Umepewa majibu* ***manne****. Chagua jibu lifaalo* **zaidi** *kati ya yale uliyopewa.*

Nyumbani kwetu __16__ miti ya kila aina. Kuna __17__ inayotupatia kivuli. Mingine __18__ mazingira __19__ mingine inatufaa kwa dawa za magonjwa mbalimbali. Ni vyema sote __20__ ili kuhifadhi miti.

**16.** A. tungepanda
B. tutapanda
C. tukipanda
D. tumepanda

**17.** A. ile
B. yale
C. zile
D. pale

**18.** A. hupambwa
B. hupamba
C. hupambika
D. hupambiana

**19.** A. angaa
B. lau
C. ilhali
D. iwapo

**20.** A. tutie fora
B. tupige chuku
C. tujitanue kifua
D. tujifunge nira

*Kutoka swali la* ***21*** *hadi la* ***30****, chagua jibu sahihi.*

**21.** Wanafunzi wana nidhamu, __________ huheshimu walimu.
A. wao
B. wewe
C. yeye
D. nyinyi

**22.** Chagua neno ambalo limeambatanishwa na **kinyume** kisichofaa.

| | | |
|---|---|---|
| A. | hakika | wasiwasi |
| B. | panda | shuka |
| C. | upole | moto |
| D. | tia | toa |

**23.** Chagua ukanusho sahihi wa sentensi ifuatayo:

Afisa wa kilimo aliwashauri wanakijiji kuhusu mbinu bora za kilimo.

A. Afisa wa kilimo hajawashauri wanakijiji kuhusu mbinu bora za kilimo.
B. Afisa wa kilimo hangewashauri wanakijiji kuhusu mbinu bora za kilimo.
C. Afisa wa kilimo hakuwashauri wanakijiji kuhusu mbinu bora za kilimo.
D. Afisa wa kilimo hatawashauri wanakijiji kuhusu mbinu bora za kilimo.

**24.** Chagua ukubwa wa sentensi ifuatayo:
Mlango wa nyumba yake unapendeza.

A. Lango la jumba lake linapendeza.
B. Mlango wa jumba lake linapendeza.
C. Lango la nyumba yake linapendeza.
D. Mlango wa nyumba yake linapendeza.

**25.** Chagua jibu lenye wingi wa sentensi ifuatayo:
Ndege amejenga kiota kwenye mti huu.

A. Ndege amejenga viota kwenye mti huu.
B. Ndege amejenga kiota kwenye miti hii.
C. Ndege wamejenga kiota kwenye mti huu.
D. Ndege wamejenga viota kwenye miti hii.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com



**Geuza ukurasa**

**26.** Ni jibu lipi linaloonyesha maana ya sentensi zifuatazo?

Mikaili hakufuata maagizo ya tabibu. Mikaili aliathirika.

A. Mikaili angalifuata maagizo ya tabibu asingaliathirika.
B. Mikaili akifuata maagizo ya tabibu hataathirika.
C. Mikaili asingalifuata maagizo ya tabibu asingaliathirika.
D. Mikaili asipofuata maagizo ya tabibu hataathirika.

**27.** Chagua jibu sahihi kujaza nafasi.
Hazina ameshinda nishani ya dhahabu ________________ .

A. daima
B. kabisa
C. tena
D. nadra

**28.** Ni kiunganishi kipi ambacho kinaunganisha sentensi zifuatazo kwa usahihi?

Jibril aliweza kutengeneza gari. Ataweza pia kutengeneza baiskeli hii.

Jibril ametengeneza gari, _________ baiskeli hii?

A. sembuse
B. kama
C. maadamu
D. bali

**29.** Ni sentensi ipi inayoonyesha huruma?

A. Simile! Mpishe bwana mdogo.
B. Oyee! Wamefunga bao la kwanza.
C. Maskini! Mbuzi wangu ameumia.
D. Jamani! Tumsikize mwalimu wetu.

**30.** Zubeda ni msanii hodari. Chagua methali utakayotumia kumhimiza kuendelea kukikuza kipawa chake ili afaidike.

A. Chanda chema huvikwa pete.
B. Haba na haba hujaza kibaba.
C. Samaki mkunje angali mbichi.
D. Ukiona vyaelea vimeundwa.

Get Free Learning Resources at www.competencebased.com

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**